
"Wale Wasiosoma Hawana Tofauti
Na Wale Wasiojua Kusoma"
~*Methali Ya Kichina*

# NATAMANI KUANZA KUSOMA VITABU

## MWONGOZO WA KUJENGA TABIA YA KUSOMA VITABU

EDIUS KATAMUGORA



New
BOOK
call: +255758594893
"Wale Wasiosoma Hawana Tofauti
Na Wale Wasiojua Kusoma"
~Methali Ya Kichina
NATAMANI KUANZA
KUSOMA
VITABU
MWONGOZO WA KUJENGA
TABIA YA
KUSOMA VITABU
EDIUS KATAMUGORA
Edius Katamugora
+255758594893


**“Wale wasiosoma hawana tofauti na wale wasiojua kusoma.”**

~Methali ya Kichina

# NATAMANI KUANZA KUSOMA VITABU

## MWONGOZO WA KUJENGA TABIA YA KUSOMA VITABU

# EDIUS KATAMUGORA



## WAKFU

Kitabu hiki nakitunuku kwa wale wote wanaopenda kusoma vitabu lakini pia kwa wale waliotamani kuanza kusoma vitabu na wakashindwa.

# SHUKRANI

Nipende kuwashukuru Keneth Mbakiza na rafiki yangu Khalifa kwa kubuni jarada la kitabu hiki.

Lakini pia nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipomshukuru rafiki yangu Ashura kwa kunipa wazo la kuwaandikia watu kitabu hiki.

Mwisho nikushukuru wewe kwa kuamua kusoma kitabu hiki, yote yakisha kusemwa nikuombe usome vitabu vyangu vingine kama, Yusufu Nina Ndoto, Barabara ya mafanikio, Namna ya Kuwa Mtaalamu, Kijana wa Maarifa na Pumba za Edius.

## UTANGULIZI

Pamoja na kuwa mwandishi wa vitabu 6 sasa na hiki kikiwa cha 7 mimi pia ni msomaji mzuri wa vitabu na makala. Nimefanya kujifunza kama sehemu ya maisha yangu na mojawapo ya kitu ninachofurahia.

Mpaka sasa nimesoma vitabu vingi sana na matokeo chanya ya usomaji wa vitabu nimeyaona. Sijawahi kujutia kupoteza hata shilingi moja kwenye kununua kitabu chochote kila kitabu nilichosoma kwa namna moja ama nyingine kimenisogeza katika hatua fulani ya kimaisha. Naweza kusema kwangu mimi dunia isiyo na vitabu ni sawa na kwamba umeninyima oksijeni. Bila vitabu siishi.

Sambamba na hayo yote nimekuwa nikiwashauri watu wengi umuhimu na faida za kusoma vitabu. Ni wachache sana wameweza kujenga tabia hii, kuna wengine ndo kabisa hawaamini lolote kuhusu vitabu ukiwaambia kusoma vitabu ni kama unawapigia kelele.

Kitabu hiki nimekiandika baada ya maombi ya wengi kuniomba niwaandikie kuhusu

umuhimu wa kusoma vitabu na namna wanavyoweza kujenga tabia ya kusoma vitabu.

Ni matumaini yangu makubwa kwamba ukisoma kitabu hiki hautakuwa na dukuduku lolote au wasiwasi kuhusu usomaji wa vitabu.

Kikubwa na cha msingi ni kwamba ukimaliza kusoma yaliyoandikwa humu kazi kubwa ni kuyaweka katika vitendo.

~**Edius Katamugora** (Aprili 13, 2020)

## 1. KWANINI UJENGE TABIA YA KUSOMA VITABU?

Siku moja mwandishi wa habari akiwa katika usaili na mwanaharakati Malcom X alimuuliza swali hili; "Ulisoma shule gani?"

Malcom X alijibu kwa sentensi fupi "VITABU"

Inawezekana umekuwa ukijiuliza watu wanaosoma vitabu wanapata faida gani au huwa wananufaika na nini. Kuna watu wengine wakilinganisha faida na hasara za kitu ndipo wanapoona thamani ya kitu.

Kabla sijataka kwenda mbali kukuingiza katika uchambuzi wa kina wa kitabu hiki naomba nikupe faida wanazozipata wanaosoma vitabu.